



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI
ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU



18 Novemba, 2022.

TAARIFA KWA UMMA

KUKANUSHA TAARIFA ZA UPOTOSHAJI.

Kumekuwepo na taarifa za uongo na upotoshaji zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii na majukwaa mengine ya habari isiyo rasmi kuwa walimu wapya 61 walioajiliwa katika Halmashauri ya Ushetu, Walalamika kuibiwa Tsh 300,000 kila mmoja.

Ukweli ni kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu, iliwalipa walimu hao wapya 61 kwa kufuata **Waraka wa Watumishi wa Serikali Na.1 wa Mwaka 2022**, ambapo kila mmoja wa walimu hao alipata sitahiki zake kama Waraka huo unavyoelekeza. Hivyo taarifa hizo zinazosambaa, Zipuuzwe kwani hazina ukweli wowote na badala yake zimelenga kuichafua taasisi ya Ushetu na Serikali kwa ujumla.

Tunaomba Umma utambue kuwa taarifa hizo za Upotoshwaji ni kinyume cha sheria na maadili ya Habari, hivyo kwa yeyote atakayehusika na usambazaji wa taarifa hiyo,

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji haitosita kumchukulia hatua za Kisheria.

Asanteni.

Emmanuel Shomary
AFISA MAWASILIANO SERIKALINI
USHETU